Wewe na Simu yako.pdf 1 06/09/2023 13:22




Kipeperushi hiki kimetayarishwa kama sehemu ya **Mpango wa Elimu kwa Mtumiaji wa Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya (CA).** Kimeandaliwa kutokana na vyanzo mbalimbali kuhusu taarifa inayopatikana kwenye simu za mkononi na kwako wewe.

## Utangulizi

Watumiaji wanafaa kufahamu haki na wajibu walio nao kuhusiana na kununua simu ya mkononi kwa kuwa wako katika hatari ya kuhadaiwa au kuuziwa bidhaa duni. Ni muhimu wajue ili wajilinde na pia wafahamu njia zote za kupata haki ikiwa haki zao zimekiukwa.

## Kununua simu ya mkononi

Kuna aina nyingi za simu za mkononi zinazopatikana, zikibainishwa kulingana na bei, ukubwa na uwezo wao. Unapochagua simu inayokufaa, unashauriwa kutafuta kwenye maduka tofauti tofauti, ili kuepuka kufanya maamuzi ya papo kwa hapo na hivyo kujilinda dhidi ya kupotoshwa na mauzo ya bei za chini kwa namna isiyo ya kawaida (ambazo zinaweza kuficha gharama au kasoro zisizo dhahiri).

## Unapaswa kuangalia nini kwenye simu ya mkononi?

Watumiaji wanapaswa kukumbuka ukweli kwamba baadhi ya vipengele vya simu za mkononi za siku hizi vinamwezesha mtumiaji:

1. Kupiga na kupokea simu, kutuma ujumbe mfupi wa maandishi, Huduma ya Ujumbe wa Maudhui Anuwai (MMS) na kupiga simu za video.
2. Ufikiaji wa data isiyotumia waya ya bendipana na ufikiaji wa tovuti kwa kutumia teknolojia za GPRS, WAP, EDGE, 3G na 4G.
3. Ukubwa na uzani wa kifaa cha simu, nafasi ya hifadhi na kasi ya simu.
4. Vitu vya ziada kama vile vifaa vya usaidizi wa kusikia na kifurushi cha kutumia kwenye gari.
5. Dhamana na masharti ya dhamana.
6. 'Muda wa kuzungumza' wa simu (muda utakaowezesha mazungumzo kwenye betri iliyotiwa chaji kikamilifu na kwenye hali bora zaidi).
7. Bei ya kifaa cha simu.

## Kuteua Mtoa Huduma za Simu

Watumiaji wanashauriwa kufanya utafiti kuhusu safu nzima ya huduma na taratibu za malipo zinazotolewa na mtoa huduma, upokezi wa simu ya mkononi kote nchini, kushushwa bei, huduma za kiwango kinacholipiwa na utaratibu wa kutafuta haki kabla ya kununua simu.

## Usalama wa Data

**Kuna mbinu mbili kuu za kuilinda data ili iwe salama, ambazo ni:**

### Kupitia kwa njia ya Kufunga Kadi ya SIM

Mbinu hii inahitaji mtumiaji kuhifadhi data kwenye kadi ya SIM na kutumia Nambari ya Kutambulisha Mtu Binafsi (PIN) kila wakati kadi ya SIM inapowekwa kwenye simu ya mkononi. Nambari za PIN kwa kawaida ni tarakimu 4, zinazofahamiwa na mwenye hiyo simu ya PEKEE.



### Kupitia kwa njia ya Kufunga simu yenyewe

*Nywila* - Ukitumia mbinu hii ya ulinzi wa data, simu ya mkononi inafungwa na inaweza tu kufunguliwa kwa kutumia nywila mahususi ili ifunguke kwa ajili ya matumizi. Wanapotunga nywila, watumiaji wanapaswa kukumbuka kwamba nywila zenye herufi 8 na zaidi ni salama zaidi kuliko zilizo na herufi 4.

Pia, watumiaji wanashauriwa kutumia mfumo uliojengwa ndani ya simu wa kuifunga ambao huja na simu nyingi za mkononi na ambao huwezeshwa baada ya muda fulani uliowekwa kuisha, kwa mfano, baada ya sekunde 30.

***Mchoro Salama*** - hii inahusisha uchoraji mahususi kwenye kiwambo unaoweza kutumika kufungua simu au baadhi ya programu zilizo kwenye simu.

***Ufunguaji kwa kutumia Sauti*** - baadhi ya simu zina sifa ya ufunguaji kwa kutumia sauti kama njia ya kulinda simu.

***Utambazaji wa Alama za Kidole*** - baadhi ya simu zina sifa inayokuwezesha kutambaza alama zako za vidole ambazo zimehifadhiwa kwenye simu. Utahitaji kutambaza kidole kile kimoja kila unapohitaji kufungua simu au kutumia baadhi ya programu.

***Utambazaji wa Mboni ya Jicho*** - Utambazaji wa mboni ya jicho ni njia ya kuweka maudhui yaliyo kwenye simu yako salama dhidi ya watu wanaopeleleza mambo ya watu. Kwa sababu hakuna mboni mbili za jicho zinazofanana na kwa kuwa haiwezekani kuziiga, kutambaza mboni zako za jicho ni mbinu iliyothibitishwa ya usalama wa simu ya mkononi.

## Kulinda simu yako ya mkononi

Ili kulinda simu yako ya isiibwe au kutumika vibaya:

- Iweke mahali salama ambapo haitaonekana.
- Wape watu unaowaamini pekee nambari yako
- Epuka kuitumia ukiwa mtaani au katika usafiri wa umma. Ikiwa unahitaji kupiga simu ukiwa kwenye eneo la umma, kuwa msiri na usimame mahali ambapo unaweza kuona pande zote za mahali ulipo.
- Ili kufunga simu yako, tumia nywila, PIN, mchoro, sauti au utambazaji.
- Unapotembea peke yako, weka simu yako katika hali 'tuli' au ya 'mtitigo pekee' ili mkirizo wa simu usiwazindue watu walio karibu yako unapopigiwa.
- Kuwa makini unapotembea huku ukiandika ujumbe.

  Usiache simu yako bila uangalizi ama kwenye eneo la umma au katika gari lako.
- Ikiwa unatumia simu ambayo imewezeshwa kutumia Bluetooth au Wi-Fi – basi weka programu ya kingarusi.
- Weka simu zako mbali ili watoto wadogo wasiweze kuzifikia.
- Epuka kutumia majina ya watu wanaoweza kutambulika kwa urahisi kama 'mama' au 'baba' kwa watu unaowasiliana nao ili kuwalinda dhidi ya simu wasizozitaka endapo simu yako itapotea au kuibwa.

## Mbinu mbadala za ulinzi wa data

Kuna aina mbili kuu za teknolojia ya simu ya : GSM (Mfumo wa Kimataifa wa Mawasiliano ya Simu za mkononi) na CDMA (Mgao wa Nambari kwa Ufikiaji kwa Wingi) - zote zikiwa zinatoa mbinu tofauti za ulinzi wa data.

## Ulinzi wa Data na simu ya mkononi ya GSM

Kila simu ya GSM ina nambari maalum ya kielektroniki yenye tarakimu 15 inayojulikana kama Utambulisho wa Kimataifa wa Kifaa cha Simu ya mkononi (IMEI), ambayo imepangwa kwenye kifaa cha simu ya mkononi na pia imeandikwa chini ya betri. Ili kufikia nambari ya IMEI, bofya *#06# na uandike nambari itakayotokea kwenye kiwambo.

Endapo simu yako ya mkononi imepotea au kuibwa, unapaswa kuwasiliana na mtoa huduma wako wa mtandao mara moja na uwape nambari ya IMEI ili waweze kuzuia simu yako ya mkononi kutumika na kadi yoyote ya SIM iliyosajiliwa kwenye mtandao wowote wa GSM nchini Kenya. Hii inatumika kama kizuizi kikali dhidi ya watu wanaoweza kuwa wezi. Endapo utapata simu yako, mtoa huduma wako wa mtandao anaweza pia kufungua simu ili kurejesha simu katika matumizi ya kawaida. Nambari za IMEI pia ni muhimu kwa polisi, ambao wanaweza kuzitumia kutambua simu zilizopotea au kuibwa.

## Ulinzi wa Data na simu ya mkononi ya CDMA

Kila simu ya CDMA ina nambari maalum ya utambulisho wa kielektroniki yenye tarakimu 8 inayojulikana kama Nambari Maalum ya Kieletroniki (ESN), ambayo inaweza kupatikana chini ya betri na hutumika sawa na nambari ya IMEI kama ilivyobainishwa hapo juu.

## Unachopaswa kufanya ikiwa simu yako ya mkononi imepotea au kuibwa

Ikiwa simu yako ya mkononi imepotea au kuibwa, unapaswa kuwasiliana na mtoa huduma wako wa mtandao mara moja, uwape nambari yako ya IMEI au ESN na uwaombe wazuie simu hiyo isitumike tena siku zijazo. Ikiwa una simu ya mkononi ya GSM, mtoa huduma wako wa mtandao atazuia kadi ya SIM na nambari yako ya IMEI ili simu yako isiweze kutumika kwenye mtandao wowote wa Kenya. Pia unapaswa kuripoti kwa polisi kwamba umepoteza au simu yako imeibwa ili wakupe nambari muhimu ya utambulisho.

## Nishati iliyofichwa ya betri

Baadhi ya simu ya mkononi zimeundwa kwa njia ya kuhifadhi kiasi fulani cha nishati ya betri kwa ajili ya matumizi ya dharura. Hii inawezeshwa kwa kubofya *3370#, ambapo simu ya mkononi itawaka tena na itaonyesha kuongezeka kwa nishati ya betri kwa kiasi fulani. Hifadhi hii itajazwa kiotomati wakati simu itawekwa chaji tena.

## Unahitaji kufahamu zaidi?

Kwa habari zaidi kuhusu mada iliyopo hapo juu au sehemu nyingine yoyote ya afya na usalama wa mitambo ya mawasiliano, tafadhali wasiliana na:

COMMUNICATIONS AUTHORITY OF KENYA
*OPENING YOUR WORLD*


**Head Office**
CA Centre, Waiyaki Way, P.O. Box 14448, Nairobi 00800
Mobile: 0703042000, Email: info@ca.go.ke
Complaints: chukuahatua@ca.go.ke
020-445 5555, 0714 455 555, 0737 455 555

**CA Western Regional Office**
1st Floor KVDA Plaza
P.O. Box 2346
Eldoret 30100
Mobile: 0703042105
Email: wro@ca.go.ke

**Central Regional Office**
Ground Floor, Advocates Plaza
P.O Box 134
Nyeri 10100
Mobile : 0703042181
Email : cero@ca.go.ke

**CA Coast Regional Office**
3rd Floor, NSSF Building
P.O. Box 8041
Mombasa 80100
Mobile: 0703042152
Email: cro@ca.go.ke

**Nyanza Regional Office**
2nd Floor Lake Basin Mall,
P.O Box 2016
Kisumu 40100
Mobile: 0703042130
Email: nro@ca.go.ke

Communications Authority of Kenya
@ca_kenya


**Ilani ya kujitoa hatarini:** Huku kila jaribio likiwa limefanywa ili kuhakikisha kuwa habari iliyojumuishwa katika hati hii ni sahihi, imekusudiwa TU kuwa kama mwongozo wa kuelekeza utendakazi salama wa mitambo ya mawasiliano na haipaswi kuchukuliwa kama (au kutumika badala ya) ushauri wa kisheria. Kwa hivyo,

Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya haitakubali kosa lolote kwa matokeo ya hatua zozote zilizochukuliwa, au maamuzi yaliyotolewa kwa misingi ya taarifa iliyotolewa.

**CA/PEA/CEP/KIS/B/10/2020**

COMMUNICATIONS AUTHORITY OF KENYA

www.ca.go.ke

# Wewe na simu yako

CHUKUA HATUA
Pata huduma ya mawasiliano unayostahili